

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



MKOA WA SIMIYU

Tel : 0282 981193

Fax : 0282 981194

Email : dedbusega@yahoo.com

Sanduku la Posta 157,
BUSEGA.

24 Agosti, 2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kwa barua ya tarehe 20 Agosti, 2018 yenye Kumb. Na. FA.170/533/01/68 kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

Kwahiylo, anawatangazia Watanzania wote wenye Sifa na uwezo wa kujaza nafasi **05** za kazi kwa kada mbalimbali kama zilivyoorodheshwa hapa chini:-

1. DEREVA II (Nafasi 04)-TGS B

SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa kidato cha IV(Form IV) na leseni ya **Daraja E** au **C1** ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundı Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Wenye cheti cha majaribio ya Ufundı Daraja la II watafikiriwa kwanza.

MAJUKUMU YA KAZI.

- Kuendesha magari ya abiria na malori
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake viro katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
- Kutunza na kuandika daftari la safari “log – book” kwa safari zote.

2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II (Nafasi 01) – TGS. B

SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha Nne au sita wenye cheti cha Utunzaji wa kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

MAJUKUMU YA KAZI.

- Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.
- Kudhibitisha upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/ nyaraka.
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk.) katika mafaili.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenyewe umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
4. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results havitakubalika**)
6. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **Wasiombe Kazi** na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
7. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe **kwa njia ya Posta** kabla ya tarehe **09/09/2018** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P. 157
BUSEGA.


Anderson Njiginya Kabuko
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
BUSEGA.

*DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
BUSEGA DISTRICT COUNCIL
BUSEGA*